



## EARL

The Elder Abuse Resource Line (EARL) ni nambari iliyo kwenye kituo cha kuhifadhi wahanga wa unyanyasaji wa wazee, na ni simu inayofanya kazi wakati wowote, kila siku, usiku au mchana (ma saa ishirini na ine). Lengo lake ni kupatiana msaada wa habari na rufaa kwa wazee katika eneo la Calgary na maeneo jirani, wanaokumbwa na unyanyasaji.

Piga simu kwa EARL kuulizia nafasi ya makazi, ikiwa wewe au mtu unayemjua anakabiliwa na unyanyasaji, au una maswali kuhusu unyanyasaji wa wazee.



# unison™

### Calgary

Kerby Centre  
1133-7 Avenue S.W.  
Calgary, AB T2P 1B2  
(403) 265-0661



[UnisonAlberta.com](http://UnisonAlberta.com)



Seniors Community & Social Services

Charitable # 11897 9947 RR0001



**unison**  
At Kerby Centre

**Usaidizi kwenye  
unyanyasaji wa  
wazee**

**Elder Abuse Supports  
Kiswahili Translation**



## Kituo cha kuhifadhi wahanga wa unyanyasaji wa wazee

Kituo chetu cha kuhifadhi wahanga wa unyanyasaji wa wazee hutoa mahali salama kwa wale wenye umri wa miaka 55 na zaidi wanaokimbia unyanyasaji.

Kwa sasa, kuna vitanda 14 vilivyofadhiliwa na kitanda kimoja cha dharura kwa rufaa za polisi. Kipindi cha wastani cha kukaa kwenye kituo ni siku 90. Tunawakaribisha wanaume na wanawake.

Tangu mwanzo wa janga la virusi ya corona, kituo kimekuwa kikiendeshwa kwa uwezo kamili na tumelazimika kukataa wazee.



Wazee wakiwa kituoni, wanapokea programu za elimu na burudani, usaidizi na maombi ya kifedha na makazi, rufaa, na mambo mengine.

Msaada wa Kijamii wa Jamii unapeanwa kwa muda wa hadi miezi 12 baada ya wateja kurudi tena katika jamii.

## Aina za Unyanyasaji wa wazee

### Kiuchmi

Matumizi haramu au yasiyofaa ya mali, fedha, au mali nyingine.

### Kihisia

Maumivu au msongo unaosababishwa kwa njia ya maneno au njia zisizo za maneno.

### Kimwili

Matumizi ya nguvu inayosababisha jeraha, maumivu, au upungufu wa uwezo.

### Kupuuzia

Kukataa au kushindwa kutoa mahitaji muhimu ya maisha

### Kutelekezwa

Kutengwa na mtu aliyejibika kwa mzee

### Kingono

Mawasiliano ya kingono yasiyoruhusiwa kwa kila namna